## KUCHANJWA KUNAKOHITAJIKA
UANGALIZI HALALI WA WATOTO

### UMRI WA MIEZI 19 HADI 23

**Dozi 4 Pneumococcal** ikiwa dozi ilipokelewa wakati au baada ya umri wa miezi 12; AU **dozi 3** ikiwa dozi 1 au zaidi ilipokelewa wakati au baada ya umri wa miezi 12; AU **dozi 2** ikiwa dozi zote mbili zilipokelewa wakati wa umri wa miezi 12 au zaidi.

**Dozi 1 Surua/Rubela**

**Dozi 1 Varicella** AU historia ya kutegemewa ya ugonjwa asilia.

### UMRI WA MIEZI 24 AU ZAIDI

**Dozi 4 Dondakoo/Pepopunda/Kifaduro**

**Dozi 3 Polio**

**Dozi 3 Hib** ikiwa dozi ilipokelewa wakati au baada ya umri wa miezi 12; AU **dozi 2** ikiwa dozi ya kwanza ilipokelewa wakati au baada ya umri wa miezi 12; AU **dozi 1** ikiwa dozi ilipokelewa wakati wa umri wa miezi 15 au zaidi. Chanjo ya Hib haihitajiki kwa watu wenye umri wa miezi 60 au zaidi.

Dozi 4 **Pneumococcal** ikiwa dozi ilipokelewa wakati au baada ya umri wa miezi 12; AU **dozi 3** ikiwa dozi 1 au zaidi ilipokelewa wakati au baada ya umri wa miezi 12; AU **dozi 2** ikiwa dozi ya kwanza ilipokelewa wakati wa umri wa au baada ya miezi 12; AU **dozi 1** ikiwa dozi hiyo ilipokelewa wakati wa umri wa au baada ya miezi 24. Chanjo ya Pneumococcal haihitajiki kwa watu wenye umri wa miaka 60 au zaidi.

**Dozi 1 Surua/Rubela**

**Dozi 1 Varicella** AU historia ya kuaminika ya ugonjwa asilia.

## Chanjo: Hatua bora kwako katika kujikinga.

Ukiwa na maswali, muulize mtoa huduma wako wa afya.

**KWA MAELEZO ZAIDI KUHUSU CHANJO NA MAGONJWA, TEMBELEA**

- **hhs.iowa.gov/public-health/immunization**
- **www.immunize.org**
- **www.cdc.gov/vaccines**
- **www.aap.org**

IOWA Health and Human Services
Public Health

09/2024

# Mahitaji ya Kuchanjwa ya Kituo cha Malezi ya Watoto Kilichopewa Leseni

Pata chanjo kwa ajili ya maisha mazuri!



IOWA Health and Human Services
Public Health

## KUCHANJWA KUNAKOHITAJIKA
UANGALIZI HALALI WA WATOTO

### CHINI YA UMRI WA MIEZI MINNE

Chati hii inajumuisha mahitaji muhimu ya kushiriki katika uangalizi halali wa watoto. Chanjo za kawaida zinaanza katika umri wa miezi 2.

### UMRI WA MIEZI 4 HADI 5

**Dozi 1 ya Dondakoo /Pepopunda / Kifaduro, Polio, Hib, Pneumococcal**

### UMRI WA MIEZI 6 HADI 11

**Dozi 2 za Dondakoo/Pepopunda/ Kifaduro, Polio, Hib, Pneumococcal**

### UMRI WA MIEZI 12 HADI 18

**Dozi 3 Dondakoo/Pepopunda/Kifaduro**

**Dozi 2 Polio**

**Dozi 2 Hib AU dozi 1** iliyopokelewa wakati wa umri wa miezi 15 au zaidi.

**Dozi 3 Pneumococcal** AU **dozi 2** ikiwa dozi zote mbili zilipokelewa wakati wa umri wa miaka 12 au zaidi.

### UMRI WA MIAKA 19 HADI 23

**Dozi 4 Dondakoo/Pepopunda/Kifaduro**

**Dozi 3 Polio**

**Dozi 3 Hib** ikiwa dozi ilipokelewa wakati au baada ya umri wa miezi 12 AU **dozi 2** ikiwa dozi ya kwanza ilipokelewa wakati au baada ya umri wa miezi 12 AU **dozi 1** ikiwa dozi ilipokelewa wakati wa umri wa miezi 15 au zaidi.

Thibitisho la Chanjo

## CHETI CHA KUCHANJWA

Cheti cha Kuchanjwa kinapaswa kutolewa kwa kituo halali cha huduma za afya za watoto ambapo mtoto atahudhuria. Ili kiwe halali, Cheti cha Kuchanjwa lazima kijumuishe jina na tarehe ya kuzaliwa kwa mtoto, tarehe ambazo chanjo zinazohitajika zilipokelewa na kutiwa sahihi na tabibu (MD au DO), msaidizi wa tabibu, muuguzi au msaidizi wa tabibu aliyeidhinishwa.

## CHETI CHA KUCHANJWA CHA MUDA

Cheti cha Muda cha Kuchanjwa kinaweza kutolewa kwa mwanafunzi ambaye anahama kutoka shule moja nchini Marekani kwenda shule nyingine au kwa mtoto ambaye ameanza kupokea chanjo, lakini hajakamilisha chanjo zote zinazohitajika kwa umri wake. Ili kuweza kustahiki kujisajili kwa muda, mtoto ni lazima apokee angalau dozi moja ya kila chanjo zinazohitajika kwa umri wake. Dozi inayofuata ya chanjo inayohitajika lazima itolewe haraka iwezekanavyo lakini sio zaidi ya siku 60 tangu kutolewa kwa dozi za(ya) awali. Ikiwa mwisho wa siku 60, mtoto atakuwa hakupokea dozi inayofuata ya chanjo inayohitajika, mtoto huyo hawezi kuhudhuria katika uangalizi halali wa watoto.



## KUTOKURUHUSIWA KUPATA CHANJO KIMATIBABU

Ruhusa ya kutopata chanjo kimatibabu inaweza kutolewa ikiwa mtoa huduma wa afya anaamini chanjo zinaweza kumdhuru mtoto. Ili kiwe halali, Cheti cha Ruhusa ya Kutokupata Chanjo Kimatibu lazima kijazwe na kutiwa sahihi na tabibu aliyepewa leseni wa Iowa (MD au DO) msaidizi wa tabibu au muuguzi aliyehitimu.

## RUHUSA YA KUTOPATA CHANJO KIDINI

Ruhusa ya kutopata chanjo kidini inaweza kutolewa ikiwa chanjo zinahitilafiana na imani ya kweli na muhimu ya kidini na sio kulingana na maoni ya kisayansi, kimatibabu au kibinafsi. Ili kiwe halali, Cheti cha Ruhusa ya Kutopata Chanjo Kidini lazima kijazwe kwa jina na tarehe ya kuzaliwa ya mtoto na kutiwa sahihi na mwenyewe binafsi au mzazi wa mtoto au mlezi.

## UTEKELEZAJI

Wanafunzi ambao hawawezi kutoa Cheti cha Chanjo, Cheti cha Chanjo cha Muda au Cheti cha Ruhusa ya Kutopata Chanjo katika siku ya kwanza hawawezi kuhudhuria kituo halali cha ungalizi wa watoto.

## REKODI ZA KUCHANJWA

Ni muhimu kuweka rekodi za kuchanjwa katika eneo salama. Thibitisho za kuchanjwa zinaweza kuwa muhimu maishani. The Iowa Department of Health and Human Services haiweki karatasi za historia ya rekodi za kuchanjwa. Hata hivyo, rekodi za kuchanjwa zinaweza kuingizwa katika Mfumo wa Sajili za Taarifa za Kuchanjwa ya Iowa (Iowa's Immunization Registry Information System, IRIS). Zungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu kuingiza uchanjwaji katika IRIS na kupata nakala ya rekodi zako.

## SHERIA YA IOWA KUHUSU KUCHANJWA

Kijitabu hiki kinaorodhesha mahitaji ya chini ya kuchanjwa kwa mtoto ili aweze kuhudhuria huduma halali za malezi ya watoto Iowa. Mahitaji haya ni kwa mujibu wa sheria ya Iowa na mapendekezo kutoka kwa Kamati ya Ushauri Kuhusu Mienendo ya Kupata Chanjo (Advisory Committee on Immunization Practices, ACIP) na ni mahitaji ya chini ya kudumisha afya ya mtoto katika mazingira ya vikundi.

Mahitaji ya kuchanjwa Iowa hutumika kwa watu WOTE wanaohudhuria vituo halali vya huduma za malezi ya watoto Iowa.

